**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

**MAMLAKA YA KUDHIBITI UNUNUZI WA UMMA**

PPRA
Public Procurement Regulatory Authority

# RIPOTI YA HALI YA UNUNUZI SERIKALINI KWA MWAKA2020/21

***(Julai 2020 - Juni 2021)***

## TOLEO LA MWANANCHI

**Novemba 2021**

YALIYOMO


Ujumbe Wa Mwenyekiti ..... iv

Ujumbe Wa Afisa Mtendaji Mkuu ..... v

Muhtasari ..... vi

Sura Ya Kwanza ..... 1

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Utekelezaji Wa Majukumu ..... 1

1.3 Matokeo Ya Utekelezaji Wa Majukumu ..... 1

Sura Ya Pili ..... 6

2.0 Tathmini Ya Ununuzi Serikalini ..... 6

2.1 Ukaguzi Wa Ununuzi Uliofanywa Kwa Njia Ya Mtandao (Taneps) ..... 6

2.2 Matokeo Ya Ukaguzi Wa Ununuzi ..... 6

2.2.1 Malengo Ya Ukaguzi ..... 6

2.2.2 Thamani Ya Tenda Zilizokaguliwa ..... 7

2.2.3 Uchaguzi Wa Taasisi Zilizokaguliwa ..... 7

2.2.4 Ukaguzi Na Matokeo Ya Uzingatiaji Wa Sheria ..... 7

Sura Ya Tatu ..... 12

3.0 Changamoto, Ufumbuzi Na Hitimisho ..... 12

3.1 Hitimisho ..... 12

## JEDWALI ZILIZOMO

Jedwali Na. 2 - 1: Taasisi zilizofanya vizuri ........ 8
Jedwali Na. 2 - 2: Taasisi zilizofanya vibaya ........ 8
Jedwali Na. 2 - 3: Taasisi zilizofanya ununuzi yenye thamani kubwa ........ 9
Jedwali Na. 2 - 4: Mikataba iliyofanyiwa ukaguzi wa kupima thamani ya fedha ........ 9
Jedwali 3 - 1: Changamoto katika ununuzi serikalini ........ 12

## Kuhusu PPRA

PPRA imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ambayo imeipa mamlaka jukumu la kusimamia ununuzi serikalini.

## Dhima

Kusimamia mfumo wa ununuzi wa umma utakaowezesha upatikanaji wa thamani bora ya fedha na matokeo yenye tija kijamii na kiuchumi

## Dira

Mfumo adilifu wa ununuzi wa umma wenye kuleta thamani bora ya fedha

## UJUMBE WA MWENYEKITI



Tangu mwaka 2006, PPRA imekuwa ikiandaa toleo maalum kwa wananchi kuhusuripoti ya tathmini ya utendakazi ya Mamlaka. Pamoja na mambo mengine,ripoti hiyo huelezea kazi zilizotekelezwa na PPRA katika mwaka husika ili kuwafahamisha wadau namna taasisi inavyotekeleza majukumu yake na jinsi taasisi nyingine za Serikali zinavyozingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali, chini ya uongozi imara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango, na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kusimamia vizuri rasilimali za taifa zikiwemo fedha za walipa kodi.

Pia, ninatoa shukrani kwa uongozi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Uongozi na Menejimenti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Msajili wa Hazina, kwa kutupatia ushirikiano ambao umeisaidia PPRA kutekeleza vizuri majukumu yake.

Baada ya hayo, napenda kuujulisha umma kuwa toleo hili maalum limeandaliwa kwa lugha rahisi ili msomaji aweze kuelewa kwa urahisi masuala ya ununuzi serikalini, yaliyojitokeza katika Ripoti ya Tathmini ya Utendakazi ya kipindi cha Julai 2020 mpaka Juni 2021.

Ni matumaini yangu kuwa Taasisi za Serikali, asasi za kiraia, wananchi na wadau wa ununuzi watatumia toleo hili siyo tu kuboresha uwazi nauwajibikaji lakini pia kuleta hamasa katika ufuatiliaji wa miradi katika maeneo yao.

Balozi Dkt. Matern Y. C. Lumbanga

## UJUMBE WA AFISA MTENDAJI MKUU



Toleo hili maalum linahusu ripotiya utendakazi wa PPRA kwa kipindi cha Julai 2020 mpaka Juni 2021, ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha tathmini yautekelezaji wa miradi ya maendeleo, utoaji wa miongozo na ushauri kwa wadau wa ununuzi, na viwango vya uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Kwa niaba ya Menejimenti na watumishi wa PPRA, ninapenda kutumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wadau wote walioiwezesha taasisi yetu kupata mafanikio yaliyoainishwa kwenye ripoti hii. Wadau hao ni pamoja na Uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango, taasisi zinazosimamia sekta ya ununuzi wa umma nchini, zikiwemo Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma (PPAA), Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), na Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA). Wadau wengine ni taasisi nyingine za Serikali, bodi zakitaaluma, wazabuni pamoja na umma kwa ujumla.

Pia, ninawashukuru wadau wengine wanaosimamia masuala ya uwajibikaji, akiwemo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma, na Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (Takukuru) kwa kushirikiana na PPRA katika kutekeleza majukumu yake.

Mwisho, ninaishukuru Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na watumishi wa PPRA kwa jitihada zao za dhati na uchapakazi unaozingatia weledi na uadilifu katika kuhakikisha malengo ya taasisi yanafikiwa.

Dkt. Irene C. Isaka

**AFISA MTENDAJI MKUU**

## MUHTASARI

Toleo hili maalum linahusu Ripoti ya Utendakazi wa PPRA, ambayo imejumuisha kazi mbalimbali za udhibiti na usimamizi zilizofanywa na PPRA kati ya Julai 2020 na Juni 2021, kwa lengo la kuboresha shughuli za ununuzi serikalini.

Sura **ya Kwanza:** Inaelezea matumizi ya TANePS, utoaji wa mafunzo kwa wadau wa ununuzi serikalini, usimamizi wa mienendo ya wazabuni, na utoaji wa huduma za ushauri kuhusiana na Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Sura **ya Pili:** Inahusu ukaguzi uliofanywa na PPRA katika taasisi za Serikali kwa kipindi cha Julai 2020 mpaka Juni 2021.

Sura **ya Tatu**: Inahusu changamoto dhidi ya PPRA katika utekelezaji wa majukumu yake, na inavyozitatua.

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Katika kuwatimizia wananchi mahitaji yao, Serikali hufanya ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma, kwa kutumia fedha zilizotengwa kwenye bajeti. Sheria ya Ununuzi wa Umma inaitaka kila taasisi ya Serikali kuandaa mpangomwaka wa ununuzi sambamba na bajeti. Pia, sheria hiyo imeweka misingi ya uwazi, ushindani na haki inayopaswa kuzingatiwa, na PPRA imepewa jukumu la kusimamia jambo hili.

## 1.2 Utekelezaji wa Majukumu

Katika kipindi cha kati ya Julai 2020 na Juni 2021, PPRA ilitekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kutoa ushauri wa masuala ya ununuzi kwa taasisi za Serikali na wadau wengine;

ii) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma;

iii) Kutoa miongozo kwa ajili ya kutekeleza shughuli za ununuzi serikalini;

iv) Kutoa mafunzo kwa taasisi za Serikali na wadau wengine ili kujenga uwezo katika utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma;na

v) Kusimamia mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao (TANePS).

## 1.3 Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu

Matokeo ya utekelezaji ni kama inavyoainishwa kwenye vipengele vinavyofuata.

### a) Mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao (TANePS)


Hadi tarehe 30 Juni 2021, jumla ya taasisi 531 zilikuwa zimeunganishwa kwenye mfumo, ikilinganishwa na taasisi 509 zilizokuwa zimeunganishwa kufikiatarehe 30 Juni 2020.

Pia, tenda 47,637 zenye thamani ya shilingi bilioni 25,815 zilipangwa kuchakatwa kupitia kwenye mfumo, lakini kati ya hizo, tenda 31,423 zilichakatwa hivyo.




Aidha, hadi tarehe 30 Juni 2021, jumla ya wazabuni 21,194 walikuwa wamesajiliwa kwenye mfumo ili waweze kushiriki kwenye tenda zinazotangazwa humo.

Vilevile, PPRA iliendelea kutoa huduma kwa wateja ambapo kwa wastani, simu 250 zilipokewa na kuhudumiwa kwa siku. Pia, PPRA ilipokea na kuhudumia takriban baruapepe 50, na wadau 75waliofika ofisini moja kwa moja kupata huduma, kwa siku.




**b) Kutoa mafunzo**

i) Kati ya Julai 2020 na Juni 2021, PPRA iliorodhesha makundi maalum 102 (wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu) na kuyachapisha katika tovuti**(www.ppra.go.tz)**ili kuwezesha makundi hayo kunufaika na tenda zilizotengwa mahsusi kwa ajili yao;

ii) Jumla ya miongozomipya kumi ya kutekeleza shughuli zaununuzi serikaliniiliandaliwa na mingine11 ilifanyiwa mapitio na marekebisho;

iii) Watumishi 646 kutoka taasisi 25 walipatiwa mafunzo ya matumizi ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, ikilinganishwa na watumishi 281 kutoka taasisi 12 waliopatiwa mafunzo hayo kati ya Julai 2019 na Juni 2020. Pia, PPRA iliandaa mafunzo maalum kwa watumishi 1,306 kutoka halmashauri 16;

iv) Watumishi 1,320 walipata mafunzo juu ya TANePS ikilinganishwa na watumishi 2,707 katika kipindi cha Julai 2019 mpaka Juni 2020. Pia, wazabuni 1,246 kutoka mikoa 18 walipatiwa mafunzo juu ya mfumo huo, ikilinganishwa na wazabuni 531 waliopatiwa mafunzo kati ya Julai 2019 na Juni 2020; na

v) PPRA iliandaa Mkutanomwaka wa Nane wa Usimamizi katika Sekta ya Ununuzi. Mkutano huo umegawanywa katika makundi mawili, ambapo kundi la kwanza hujumuisha wajumbe wa bodi za wakurugenzi, wakuu

wa taasisi na madiwani. Kundi la pili hujumuisha wajumbe wa bodi za zabuni, watumishi kutoka idara tumizi pamoja na vitengo vya sheria, ukaguzi wa ndani, na usimamizi wa ununuzi.

Mkutano huo uliwapatia washiriki uelewa kuhusu utekelezaji wa sheria na changamoto zilizopo kwenye sekta ya ununuzi. Jumla ya washiriki 463 kutoka taasisi 133 walihudhuria mkutano huoikilinganishwa na washiriki 216 waliohudhuria kati ya Julai 2019 na Juni 2020.

**c) Kusogeza huduma karibu na wadau**

PPRA ilitumia njia mbalimbali katika kutoa elimu kuhusiana na huduma zinazotolewa na Mamlaka, ikiwa ni pamoja na matumizi ya TANePS na Sheria ya Ununuzi wa Umma. Miongoni mwa njia hizo ni matumizi ya vyombo vya habari kama vile televisheni, redio na mitandao ya kijamii pamoja na kushiriki kwenye matukio na maonesho makubwa, yakiwemo Sabasaba na kongamanomwaka la wahandisi. Pia, PPRA ilishiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu.

**d) Usimamizi wa mienendo ya wazabuni**

Sheria ya Ununuzi wa Umma imeipa PPRA nguvu ya kufungia wazabuni ili wasishiriki kwenye tenda za serikali kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo ukiukwaji masharti ya mkataba, vitendo vya rushwa au udanganyifu katika mchakato.
Kati ya Julai 2020 na Juni 2021, PPRA ilipokea jumla ya mapendekezo 24 ya kufungia wazabuni. Mapendekezo 16 kati ya hayo, yalikataliwa kwa sababu ya kuwasilishwa nje ya muda, na matano yalikataliwa kwa kukosa sababu za msingi. Pia, PPRA iliifungia kampuni moja kwa kipindi cha miaka 10 kutokana na kile kilichoonekana kuwa ilikuwa imefanya udanganyifu. Hata hivyo, kampuni hiyo iliondolewa kifungo na Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma (PPAA) baada ya kushinda rufaa.

**e) Kuwafikia wadau**

Kati ya Julai 2020 na Juni 2021, PPRA iliendelea kutoa taarifa za ununuzi kama inavyoelezewa katika sehemu zinazofuata.

### i) Jarida la ununuzi

Jarida la ununuzi *Tanzania Procurement Journal,* au *TPJ,* hutoa taarifa mbalimbali za ununuzi serikalini. Kati ya Julai 2020 na Juni 2021, PPRA iliandaa matoleo manne ya TPJ na kuyachapisha kwenye tovuti yake.

### ii) Elimu kwa umma

PPRA ilirusha matangazo ya redio na televisheni kuhusu uadilifu na madhara ya rushwa katika ununuzi serikalini,Sheria ya Ununuzi wa Umma, pamoja na matumizi ya mfumo TANePS. Pia, PPRA iliendelea kutumia mitandao yake ya kijamii ambayo ni *Twitter (PpraTanzania), Facebook (PPRA_Tanzania)* na*Instagram (ppra_tanzania)* kutoa taarifa na elimu kwa umma, ambapo jumla ya taarifa 178 ziliwekwa kwenye mitandao hiyo.



# SURA YA PILI

## 2.0 Tathmini ya ununuzi serikalini

### 2.1 Ukaguzi wa ununuzi uliofanywa kwa njia ya mtandao (TANePS)

Majukumu ya PPRA ni pamoja na kupima kama Sheria ya Ununuzi wa Umma inazingatiwa na taasisi za Serikali na wadau wengine wa ununuzi.

PPRAimebaini kuwa taasisi 130 kati ya 718 zilizokuwa zimeunganishwa kwenye mfumo TANePS, hazikutumia mfumo huo, kinyume na matakwa ya sheria.




Sheria ya Ununuzi wa Umma inaitaka kila taasisi kuwasilisha PPRA taarifa za utekelezaji wa sheria hiyo.Kati ya Julai 2020 na Juni 2021 PPRA ilibaini kuwa taasisi nyingi hazikuwasilisha taarifa hizo.

### 2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Ununuzi

#### 2.2.1 Malengo ya ukaguzi

Sheria ya Ununuzi wa Umma inaipa PPRA mamlaka ya kufanya ukaguzi juu ya mchakato wa ununuzi,yaani tangu mchakato wa tenda mpaka kukamilika kwa mkataba ili kupima uzingatiwaji wa sheria na kama miradi ilileta matokeo yaliyokusudiwa. Miradi hii ni kama vile ujenzi wa barabara, daraja, shule, hospitali, miundombinu ya maji.

### 2.2.2 Thamani ya tenda zilizokaguliwa

Kati ya Julai 2020 na Juni 2021, PPRA ilifanya ukaguzi katika tenda8,838 zenye thamani ya shilingi bilioni 9,200 kutoka katika taasisi 86,ikiwemo miradi ya ujenzi 406 zenye jumla ya thamani ya Shilingi bilioni 8,027.

### 2.2.3 Uchaguzi wa taasisi zilizokaguliwa

PPRA ilizikagua taasisi ambazo zilikuwa na ununuzi wenye thamani kubwa, zile zilizokuwa zimehusishwa na ukiukwaji wa sheria,zile zilizopata maksi za chini katika ukaguzi uliopita,pamoja nazile ambazo hazikuwa zimekaguliwa kwa muda mrefu.

### 2.2.4 Ukaguzi na matokeo ya uzingatiaji wa Sheria

Ukaguzi ulilenga kupima iwapo michakato ya tenda ilizingatia Sheria. Pia, ukaguzi ulilenga tenda zenye gharama kubwa pamoja na zile zilizokuwa na uwezekano wa kupoteza fedha za Serikali.

#### i) Matokeo ya uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma

Wastani wa jumla, wa uzingatiaji wa sheria kwa taasisi 85 zilizokaguliwa,ulikuwa asilimia 75ikilinganishwa na 79 kwa mwaka uliopita.Wastani huu ni wa kuridhisha - pamoja na kwamba ulishuka ukilinganisha na mwaka uliotangulia.

Uchambuzi unaonesha kuwa, katika taasisi zote zilizofanyiwa ukaguzi, 33 zilipata wastani mzuri (yaani asilimia80 au zaidi), taasisi 47 zilipata wastani wa kuridhisha (kati ya asilimia 60 na79) wakati taasisi tano zilipata wastani hafifu (yaani chini ya asilimia 60).

Aidha, matokeo ya ukaguzi huu yanaonesha kwamba taasisi 15 zilizochakata tenda zake ndani ya mfumo TANePS, zilipata wastani mzuri (asilimia 80) ikilinganishwa na asilimia 73 kwa taasisi 41 ambazo zilichakata tenda zote nje ya mfumo huo.

**Jedwali Na. 2 - 1**: Taasisi zilizofanya vizuri

| Na. | Taasisi | Maksi (%) | Na. | Taasisi | Maksi (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mfuko wa Hifadhi kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) | 94 | 6. | Wizara ya Fedha na Mipango | 87 |
| 2. | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 93 | 7. | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) | 87 |
| 3. | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) Makao Makuu | 91 | 8. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha | 86 |
| 4. | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 91 | 9. | Wakala wa Nishati Vijijini (REA) | 86 |
| 5. | Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) | 90 | 10. | Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) | 86 |

**Jedwali Na. 2 - 2**: Taasisi zilizofanya vibaya

| Na. | Taasisi | Maksi (%) |
|---|---|---|
| 1 | Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe | 51 |
| 2 | Halmashauri ya Mji wa Kondoa | 49 |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo | 58 |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya ya Chato | 51 |
| 5 | Taasisi ya Utafiti wa Wanyama | 53 |

### ii) Matokeo ya ukaguzi wa ununuzi wenye thamani kubwa

PPRA ilikagua taasisi 16 ambazo zilifanya ununuzi wenye thamani kubwa na kubaini kuwa uzingatiaji wao wa sheria ulikuwa wa wastani wa asilimia 80 ambao ni mzuri. Thamani ya tenda zilizokaguliwa kwenye taasisi hizo ilikuwa takriban Shilingi bilioni 8,527. **Jedwali Na. 2** linaonesha orodhaya taasisi zilizofanya ununuzi mkubwa kati ya Julai 2020 na Juni 2021.

**Jedwali Na. 2 - 3: Taasisi zilizofanya ununuzi yenye thamani kubwa**

| Na. | Taasisi | Na. | Taasisi |
|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 9 | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) Makao Makuu |
| 2 | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tasac) | 10 | Wizara ya Mambo ya Ndani |
| 3 | Mahakama ya Tanzania | 11 | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| 4 | Mfuko wa Hifadhi kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) | 12 | Shirika la Nyumba Tanzania |
| 5 | Hospitali ya Mifupa (MOI) | 13 | Bohari ya Dawa (MSD) |
| 6 | Tanroads Kilimanjaro | 14 | Shirika la Reli |
| 7 | GASCO | 15 | Tanesco Makao Makuu |
| 8 | NSSF | 16 | Tanroads Makao Makuu |

### iii) Upatikanaji wa thamani ya fedha katika miradi

#### a) Ukaguzi wa kupima thamani ya fedha

PPRA ilifanya ukaguzi katika miradi 282 yenye jumla ya thamani ya takriban Shilingi bilioni 5,752 ili kupima matumizi sahihi ya fedha katika ununuzi.Ukaguzi huu ulihusisha tenda za ujenzi ikiwemo ujenzi wa barabara, madaraja, majengo na miundombinu ya maji. Pia, ukaguzi ulihusisha tenda za vifaa na za huduma mbalimbali. Mchanganuo wa Tenda zilizokaguliwa ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali 2 - 4**.

**Jedwali Na. 2 - 4**: Mikataba iliyofanyiwa ukaguzi wa kupima thamani ya fedha

| Aina ya tenda | Idadi ya miradi | Thamani (shilingi bilioni) |
|---|---|---|
| Kazi za ujenzi wa majengo | **38** | **215** |
| Ujenzi wa barabara na madaraja | **28** | **103** |
| Kazi za umeme (electrical works) | **4** | **162** |
| Ujenzi wa reli | **1** | **4,444** |

| Aina ya tenda | Idadi ya miradi | Thamani (shilingi bilioni) |
|---|---|---|
| Miradi ya maji na umwagiliaji | **5** | **9** |
| Bidhaa | **133** | **789** |
| Huduma za ushauri mbalimbali | **73** | **30** |
| **Jumla** | **282** | **5,752** |

b) **Matokeo ya ukaguzi wa upatikanaji wa thamani ya fedha**

Wastani wajumla katika ukaguzi wa kupima matumizi sahihi ya fedha katika taasisi 54 zilizokaguliwa,ulikuwa asilimia 85 ambao ni wastani mzuriikilinganishwa na mwaka uliotangulia ambao kiwango chake kilikuwa asilimia 82 kwa taasisi 62 zilizokaguliwa.

Kati ya miradi iliyokaguliwa ili kupima matumizi sahihi ya fedha, miradi 242 ilipata wastani mzuri, 39 ilipata alama za kiwango cha kuridhisha na mradi mmoja ulipata wastani usioridhisha, ambao ulitekelezwa na iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

**iv) Tathmini ya utengaji wa asilimia 30 ya bajeti ya manunuzi kwa ajili ya ushirikishwaji wa makundi maalum**

Sheria ya Ununuzi wa Umma inaitaka kila taasisi kutenga asilimia 30 ya bajeti yake ya ununuzi kwa ajili ya makundi maalum yaani wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu. PPRA ilifanya ukaguzi ili kupima endapo taasisi hizo zilitekeleza matakwa hayoya sheria.


Ukaguzi huu ulibaini kuwa kati ya taasisi 86 zilizofanyiwa tathmini hii, ni taasisi mbili tu zilizozingatia matakwa haya, taasisi tatu zilikuwa zimetengapungufu ya asilimia 30, wakati taasisi 81 hazikuwa zimetengachochote.

**v) Udanganyifu na viashiria vya rushwa**

PPRA inayo makubaliano na Takukuru juu ya kubadilishana taarifa kwa lengo la kudhibiti rushwa katika ununuzi serikalini. Kati ya Julai 2020 na Juni 2021, masuala

ya rushwa katika tenda za Serikali yalifuatiliwa katika taasisi zilizokaguliwa kwa kuzingatia makubaliano hayo.

Tathmini ya jumla ya viashiria vya rushwa ilionesha kwamba jumla ya tenda tatu zenye thamani ya shilingi milioni 617zilibainika kuwa na kiwango kikubwa cha viashiria vya rushwa.Kwa mujibu wa makubaliano, PPRA itawasilisha taarifa ya taasisi hizi Takukuru.




### vi) Uchunguzi wa tuhuma za ukiukwaji sheria

PPRA ina pia mamlaka ya kufanya ukaguzi maalum kuhusu tuhuma za ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma.Ukaguzi huu unaweza kutokana na maelekezo kutoka serikalini, taarifa kutoka kwa wasamaria wema au PPRA yenyewe inapoona inafaa. Kati ya Julai 2020 na Juni 2021, PPRA ilifanya ukaguzi maalum katika taasisi nane, ukihusisha tenda 5,530 zenye thamani ya Shilingi bilioni 207. Ukaguzi huu ulibainisha kwamba:

i) Serikali ingeokoatakriban shilingi bilioni moja endapo mapendekezo yaliyotolewa na PPRA katika ripoti yake yangezingatiwa; na pia,

ii) Serikali ilipata hasara ya takriban shilingi milioni 580kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya wazabuni, uwepo wa pembejeo zilizofikia ukomo wa muda wa matumizi, pamoja na udhaifu mwingine katika usimamizi wa tenda.

Aidha, kutokana na upungufu uliobainika, pamoja na mambo mengine, PPRA ilipendekeza hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa wale waliokiuka sheria.

## SURA YA TATU

## 3.0 Changamoto, ufumbuzi na hitimisho

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, PPRA ilikabiliwa na changamoto mbalimbali katika kusimamia ununuzi, kama inavyoainishwa katika **Jedwali Na. 3 – 1.**

**Jedwali 3 - 1: Changamoto katika ununuzi serikalini.**

| | Changamoto | Ufumbuzi |
|---|---|---|
| 1 | Taasisi nyingi kutowasilisha ripoti mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye Sheria yaUnunuzi wa Umma, hali inayoikwamisha PPRA katika utekelezaji wa majukumu yake. | PPRA itaendelea kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma pamoja na kuchukulia hatua stahiki kwa taasisi zinazokiuka matakwa hayo ya Sheria. |
| 2 | Uelewa mdogo wa wadau juu ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Kanuni namiongozo yake pamojana jinsi ya kuutumia mfumo wa TANePS. | Kuongezajuhudi za kuwajengea uwezo wadau kuhusu Sheria, Kanuni namiongozo pamoja na matumizi sahihi ya mfumo wa TANePS. |
| 3 | Baadhi ya watumishi wa Serikalina wazabuni kukosa uadilifu. | Kuimarisha ufuatiliaji na uwajibishaji wa watumishi na wazabuni wasio waadilifu. |
| 4 | Baadhi ya wazabuniwenye mikataba ya manunuzikutokuwa na uwezo wa kutimiza majukumu yaokimkataba. | Kuchukua hatua stahiki za kisheria ikiwemo kuwafungia wazabuni kutoshiriki katika tenda za Serikali pale ambapo wanashindwa kutimiza majukumu yao ya kimkataba. |
| 5 | Baadhi ya taasisi za Serikali kutofanyia kazimaelekezo yanayotokana na ukaguzi mbalimbali zilizofanywa na PPRA. | Kuchukua hatua stahiki dhidi ya taasisi za Serikalizinazokiuka utekelezaji wa maelekezoya PPRA. |

### 3.1 Hitimisho

Ripoti hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa elimu zaidi kwa wananchi wa kawaida kuhusu shughuli zilizotekelezwa na PPRA katika kusimamia ununuzi ndani ya Serikali, kama ambavyo zimeelezewa kwa kina katika ripoti ya utendakazi wa PPRA kwa kipindi cha Julai 2020 mpaka Juni 2021.

PPRA inaamini kuwa ripoti hii itamsaidia msomaji kuelewa vizuri kazi zilizotekelezwa katika mwaka husika, mafanikio, changamoto na ufumbuzi wake. Ni matumaini yetu

kuwa ripoti hii itahamasisha wananchi kuendelea kushirikiana na PPRA ili kuhakikisha kuwa ununuzi serikalini unafanywa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.